OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

SHULE YA SEKONDARI LIZABONI

S.L.P 518

SONGEA

16/12/2020

KUMB. NA LIZSS/USJ/VOL …….

MZAZI / MLEZI WA ……..

S.L.P ……

SONGEA.

YAH: **MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA KWANZA**

MWAKA 2021

Ninafurahi kukujulisha kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Lizaboni iliyoko katika kata ya Mjimwema karibu na kituo cha afya cha Mjimwema tarafa ya Songea Magharibi shule hii ni ya kutwa

- Shule itafunguliwa tarehe 11/1/2021 saa 1:00 Asubuhi kwa muhula wa kwanza. Unatakiwa umlete mototo wako shuleni siku hiyo bila kukosa. Mwanafunzi atakaye kuja bila mzazi / mlezi atarudishwa amfuate mzazi / mlezi wake hivyo usajili wake hauta fanyika kwa siku hiyo
- Mzazi / mlezi anatakiwa amwandalie mwanae mahitaji yake mapema ili aweze kuwahi masomo

1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE YA SHULE

A: WAVULANA

Sare ya shule hii ni suruali na sketi rangi ya udongo na shati jeupe mikopo mifupi, jozi mbili (kitambaa cha suruali kimeambatishwa)

- Viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi jozi mbili vyenye visigino vifupi, viwe na gidamu na visiwe wazi, raba haziruhusiwi
- Mkanda mweusi wenye upana wa nchi moja (01)
- Soksi nyeusi jozi 3

- ❖ Tai inayofanana na suruali
- ❖ Sweta la kufuma la rangi ya kijivu lenye shingo ya V lenye mstari mweupe kifuani
- ❖ Picha nne passport size za rangi
- ❖ Suruali iwe na mifuko mitatu na mkunjo wajuu **(turn up**) miguuni na malinda mawili kwenye mifuko ya mbele (**suruali iwe na upana wa sentimeta 17**)

B: WASICHANA

- ❖ Sketi ya rangi ya udongo yenye upana wa mkanda usizidi sentimeta tano (5) na iwe na urefu usiogusa viatu kwa sentemeta 18 na shati jeupe mikono mifupi jozi mbili (kitambaa cha sketi kimeambatishwa)
- ❖ Viatu vya ngozi jozi mbili vyenye visigino vifupi viwe na gidamu (viatu vya lastiki "bajaji" na raba haviruhusiwi)
- ❖ Soksi jozi tatu (3) nyeupe (isiwe na rangi mbili)
- ❖ Tai inayofanana na sketi
- ❖ Sweta rangi ya kijivu lenye shingo ya V na lenye mstari mweupe kifuani
- ❖ Picha nne passport size za rangi
- ❖ Hijabu nyeupe kwa wanohusika isiwe ndefu kuvuka viwiko vya mikono

1.1 ADA NA MICHANGO MENGINE

Sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 na ilani ya uchaguzi ya CCM – 2015 – 2020 ibara ya 52 (a) imebainisha kwamba serikali itatoa elimu ya awali na elimu msingi bure (darasa la I hadi kidato cha IV) bila malipo kuanzia mwaka wa masomo 2016.
Michango yote iliyokuwa inatozwa shuleni kutoka kwa wazazi / walezi imefutwa

1.2 MAJUKUMU YA MZAZI

- Sare ya michezo (utapewa maelezo siku ya kufungua)
- Madaftari makubwa 11, mkebe wa hesabu na kalamu
- Chakula (utapewa melekezo siku ya kufungua shule)
- Nauli ya kwenda na kurudi shuleni (kwa wanao kaa mbali)
- Matibabu
- File la mwanafunzi

Wazazi kama sehemu ya wananchi na jamii wanayozunguka shule watashiriki katika kazi ya ujenzi wa miundombinu ya shule kwa kuchangia nguvu zao au fedha kadiri itakavyoamuriwa na kijiji/ mtaa/ kata, tarafa na halmashauri \

1.3 UTARATIBU WA WIKI

Utaratibu wa kila siku, mwanafunzi ataripoti shuleni saa 1: 00 na kurudi nyumbani saa 11:00 jioni. Masomo yataanza saa 2:00 asubuhi. Ikitokea kwa bahati mbaya mwanafunzi akiwa mgonjwa taarifa itumwe shuleni. Punde atakapokuja shuleni ahakikishe anakuja na vyeti vya matibabu na kumwonesha mwalimu wa darasa

- **Utoro ni kosa lisilovumilika**

1.4 VIFAA VYA KUFANYIA KAZI

Tunaomba mwanafunzi atakapokuja kuripoti shuleni aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya kufanya usafi:

- Kila mwanafunzi atatakiwa kuja na fagio ambao atatumia kufanyia usafi na kurudi nao nyumbani

1.5 TANBIHI

I. Shule hii bado inaendelea kujengwa hivyo mzazi / mlezi tushirikiane kuikamilisha kama tutakavyo kubaliana katika vikao husika

II. Wanafunzi wote watapata chakula cha mchana hapa shuleni kutokana na michango ya wazazi / walezi kadiri itakavyokubaliwa katika vikao na watarudi nyumbani saa 11:00 jioni

III. Wanafunzi wenye magonjwa ya kudumu waje na kopi za vyeti vinavyoonesha matatizo waliyo nayo ili tuweze kuwatambua. Au mzazi / mlezi njoo shuleni (ofisini) utoe taarifa

1.6 VIAMBATISHO

Pamoja na maelekezo haya tumeambatisha viambatisho vifuatavyo ambavyo mwanafunzi atakuja navyo vikiwa vimekamilika

I. Kiambata A sheria na kanuni za shule. Azisome na kuzielewa

II. Kiambata B ijazwe na mzazi/ mlezi na pia mwanafunzi ajaze sehemu yake

III. Kiambata C kwa ajili ya vipimo vya hospitali. Mwanafunzi apimwe hospitali ya Mjimwema (kata ya Mjimwema) na ijazwe kikamilifu.

Jumuiya ya shule ya sekondari Lizaboni inakukaribisha kwa furaha katika shule. Nakutakia maandalizi mema tayari kwa kujiunga na shule ya sekondari Lizaboni

ELIMU NI UKUMBOZI

KARIBU SANA

……

LILIAN STANLEY SIMKANGA
MKUU WA SHULE

KIAMBATISHO A

KANUNNI NA SHERIA ZA SHULE

KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUZISOMA SHERIA HIZI KWA MAKINI NA AZITEKELEZE

1. WANAFUNZI

i. Sharti wasimame na kuwasalimu kwa adabu mwalimu au mtu yeyote aliyewazidi umri anapopita au anapoingia mahali walipo wanafunzi
ii. Wawapokee walimu/ wageni wanao ingia shuleni
iii. Wasitumie lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu na watu wengine
iv. Waheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama wazazi wao: uhusiano wa mwanafunzi kwa walezi wao ni ule wa mototo na baba au mama yake
v. Washirikiane, wapendane na kusaidiana wao wenyewe katika mambo mbalimbali ya masomo na wathamini na kuziheshimu kazi za aina zote
vi. Wathamini muda wa kuwahi katika shughuli zote za shule zilizopo kwenye ratiba ya kila siku kila mmoja awahi na ahudhurie wito wa dharura (emergence) waitike wito au ishara ya kuwaita bila kuchelewa
vii. Wathamini na kuheshimu mali binafsi na mali ya umma
viii. Waheshimu bendera ya taifa. Picha za viongozi wa serikali, nembo ya taifa, wimbo wa taifa na fedha za taifa
ix. Wanapokuwa darasani kwenye mikutano. N.k wanyooshe mkono juu na kusimama wanapouliza au kujibu swali
x. Wakae kimya wakati wote wanapokuwa darasani, wasitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliopo
xi. Waoneshe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahari popote
xii. Wanafunzi watatakiwa kuwa safi kimwili na kimavazi na kitabia. Mavazi ya kihuni hayatakiwi hapa shuleni

2. A. NI MARUFUKU

i. Kuvuta sigara ya aina yoyote au bangi
ii. Kushiriki aina yeyote ya ulevi
iii. Kufuga kucha ndevu. Kuwa na nywele zilizowekwa dawa kupaka **ina**, kusuka, kupaka wanja, poda, kunyoa mitindo mbali mbali ya nywele,kunyoa nyusi na kufuga ndevu.
iv. Awe na nywele ndefu (awe na nywele fupi njiti ya kiberiti ikichomekwa kwenye nywele ionekane)
v. Kuvaa mavazi yasiyokuwa ya heshima
vi. Kuzurura ovyo

vii. Kugombana na wenzako au mtu yoyote matusi na uonevu wa aina yeyote umepigwa marufuku
viii. Kuwa na simu ya mkononi

NB; Tafadhali mshauri mwanao azingatie na kufuata sheria za shule kwa manufaa ya maendeleo yake.

B. **TAALUMA**

Mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya masomo na kufanya mazoezi Yote anayopewa na mwalimu husika. Asipofanya hivyo atapewa adhabu.

C. **KUTEMBELEA SEHEMU ZIFUATAZO ISIPOKUWA KWA KIBALI MAALUMU**

i. Chumba cha walimu na ofisi za shule
ii. Maabara
iii. Jokoni
iv. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu

D. **KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE ISIPOKUWA KWA KIBALI MAALUMU**

E. **KUTOHUDHURIA**

I. vipindi vya masomo ndani na nje ya darasa
ii. Michezo na kazi zote za mikono
iii. Baraza la shule, kupandisha bendera ya taifa, ukaguzi wa usafi n.k

F. **NI MWIKO KABISA KWENDA AU KUONEKANA KWENYE ZIFUATAZO**

i. Vilabu vya pombe pamoja na bar
ii. Majumba ya starehe
iii. Majumba ya kufikia wageni (gest house)

3. Wanafunzi wanapaswa kuwahi katika shughuri zote za shule kama zinavyopangwa kwenye ratiba ya shule ya kila siku

4. SARE YA SHELE

A. Sare ya shule ni kama ilivyoelekezwa kwenye maelezo ya kujiunga na shule hivyo kila mwanafunzi SHARTI avae sare ya shule iliyo safi na nadhifu wakati wote
   i. Wakati wa masomo darasani
   ii. Anapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule

iii. Wakati wa muhadhara wa shule (baraza la shule)
iv. Anapokwenda hospitali
v. Wakati wa maandamano
- **Sketi fupi, shati fupi na la kubana au suruali fupi na ya kubana haviruhusiwa**

B. Sare ya shule isivaliwe na vitu vifuatavyo
Kofia, Heleni, Bangili, Viatu vya ghorofa, pete, vibanio vya nywele,.

5. YAFUATAYO NI MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA

i. Wizi
ii. Uasherati, ubakaji na ushoga
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
iv. Makosa ya jinai
v. Kupiga na kupigana
vi. Kuharibu kwa makusidi mali ya uma
vii. Kudharau bendera ya taifa
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kupata mimba au kusababisha mimba nje na ndani ya shule
x. Kutoa mimba
xi. Kogoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga Amani na usalama wa watu
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xiii. Kutua au kutumia lugha ya matusi

6. TANBIHI

Mwanafunzi anapata msamaha wa kutofanya kazi za nje iwapo ana cheti cha daktari kinachothibitisha asifanye kazi

KIAMBATISHO B

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU

SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi …….. naikubali nafasi niliyoipata katika shule ya sekondari Lizaboni kuendelea na masomo. Ninakiri kuwa nitasoma kwa faida yangu na taifa langu kwa ujumla

Naahidi mbele ya mzazi / mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa upeo na uwezo wangu wote kuwa mwanafunzi mwema. Naahidi kutoshiriki katika mambo yatakayosababisha mwanafunzi kuachishwa masomo. Naahidi kuwa nitashirikiana na walimu pamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa shule na taifa kwa ujumla

Sahihi ya mwanafunzi …… Tarehe ……

SEHEMU YA MZAZI

Mimi …….. nimesoma yote na kuyaelewa. Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyotajwa katika fomu ya kujiunga na shule. Ripoti na barua zote zinazo muhusu mwanafunzi huyu ziletwe kwangu kwa anwani hii
……
……

Jina la mzazi / mlezi……
Sahihi ……..
Tarehe ……
Namba ya simu ……..

KIAMBATISHO C

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRIME MINISTER OFFICE

SHULE YA SEKONDARI LIZABONI
P. O BOX 518
SONGEA
……../……../ 20…...

MEDICAL OFFICER
…….
……
……..

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR…….……

Please examine the above named as to his/her fitness as indicated below. Arrange for necessary examination so that the certificate may be signed and brought to school by the student. This certificate must be signed by a qualified medical officer from a recognized hospital

Thank you in advance.

……

MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above named student with regard to: -

Skin……	Abdomen …….
Eyes……	Urine ……
Teeth ……..	Hemoglobin …….
Speech ……	Chest ……
Heart ……..	Blood pressure …….
Blood group …….	Pregnancy ……

Any physical and mental disability ……

Do you, therefore, recommend the named student medically fit for studentship at this school?

……

……

NAME …….SIGNATURE AND STAMP……

STATION…….DESIGNATION ……